

# Sherehe ya Maombi ya Dunia 2025

**Sifa**—Mungu ni Mshindi; aliyeyashinda na kumshinda adui.

1 Nyakati 29:11 (SUV) Ee BWANA, ukuu ni wako, na uweza, na utukufu, na kushinda, na enzi; maana vitu vyote vilivyo mbinguni na duniani ni vyako; ufalme ni wako, Ee BWANA, nawe umetukuzwa, u mkuu juu ya vitu vyote.

Zaburi 98:1 (SUV) Mwimbieni BWANA wimbo mpya, kwa maana ametenda mambo ya ajabu. Mkono wa kuume wake mwenyewe, Mkono wake mtakatifu umemtendea wokovu.

Mithali 21:31 (SUV) Farasi huwekwa tayari kwa siku ya vita; Lakini BWANA ndiye aletaye wokovu.

1 Korintho 15:57-58 (SUV) Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo. Basi ndugu zangu wapendwa, mwimarike, msitikisike, mkazidi sana kutenda kazi ya Bwana siku zote, kwa kuwa mwajua ya kwamba taabu yenu siyo bure katika Bwana.

**Muongamo**—1 Yohana 1:9 (SUV) Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.

**Shukurani**—Zaburi 20:5 (SUV) Na tuushangilie wokovu wako, Kwa jina la Mungu wetu tuzitweke bendera zetu. BWANA akutimizie matakwa yako yote.

## Maombezi—

**Watoto:** Naomba \_\_\_\_\_ awe na Imani isiyo ya hekima ya wanadamu, bali katika nguvu za Mungu.

Kutoka 1 Korintho 2:5 SUV

**Wasiyo wakristo:** Naomba \_\_\_\_\_ ajue kuwa hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo.

Kutoka Matendo ya Mitume 4:12 SUV

**Walimu:** Naomba \_\_\_\_\_ asitoe neno lo lote lililo ovu kinywani mwake, bali lililo jema la kumfaa mwenye kuhitaji, ili liwape neema wanaosikia.

Kutoka Efeso 4:29 SUV

**Shule:** Mungu asikie huko mbinguni, akisamehe dhambi za watumwa wake, na Shule ya \_\_\_\_\_ kweli; afundishe shule ya \_\_\_\_\_ njia iliyo njema ipasayo kuiendea.

Kutoka 1 Wafalme 8:36a SUV

**Wamama Katika Maombi (MIP):** Naomba Mungu awajaze kila Mama katika Maombi wanachohitaji kwa kadiri ya utajiri wake Yesu Kristo.

Kutoka Wafilipi 4:19 SUV

**Baraka:** Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, na upendo wa Mungu Baba, na ushirika wa Roho Mtakatifu, ukae nasi sote.

2 Korintho 13:14 SUV



Wamama Waombezi Kimataifa